MARIE MCAULIFFE
BINOD KHADRIA

1 MUHTASARI WA RIPOTI: KUTOA TASWIRA YA UHAMIAJI NA MWENDO KATIKA NYAKATI ZENYE MASHAKA MENGI[1]

Utangulizi

Kusanyiko la ushahidi wa muda mrefu na unaokua wa uhamiaji na mwendo unaonyesha kuwa uhamiaji kwa kiasi kikubwa unahusiana na mabadiliko mapana ulimwenguni ya kiuchumi, kijamii, kisiasa na kiteknolojia ambayo yanaathiri maswala anuwai ya sera yenye kipaumbele cha juu.[2] Jinsi michakato ya utandawazi inavyozidi kuongezeka, mabadiliko haya yanazidi kuathiri maisha yetu - katika mahali petu pa kazi, katika nyumba zetu, katika maisha yetu ya kijamii na kiroho - tunapoendelea na shughuli zetu za kila siku. Watu wengi zaidi wanaweza kupata habari, bidhaa na huduma kutoka ulimwenguni kote kwa sababu ya upanuzi unaoendelea katika teknolojia za kupunguza umbali.

Kuna hisia pia kwamba tuko katikati ya kipindi cha mashaka makubwa. Watoa maoni wengi wametilia shaka uthabiti wa vipengele vya utaratibu wa kisiasa ulimwenguni uliobuniwa punde baada ya vita vikuu viwili vya dunia, pamoja na jinsi vinahusiana na ushirikiano baina ya nchi na masilahi ya pamoja.[3] Wengine wanauita wakati huu "kipindi cha hasira", wakifuatilia chanzo cha hali ya sasa ya mashaka katika siasa za kijiografia na kutoridhika hadi kwa uzingatiaji uliotawala na usiopungua kuhusu "mantiki" na "urazini huru" badala ya mwitiko wa kihisia.[4]

Ni katika muktadha huu ambapo ripoti hii ya uhamiaji duniani inazingatia maendeleo ya uhamiaji katika kipindi cha miaka miwili iliyopita, ikiweka msisitizo kwenye utoaji wa uchambuzi unaozingatia maslahi ya kihistoria na kisasa. Ni ya kihistoria kwa kutambua kwamba uhamiaji na ufurushwaji hutokea katika miktadha mipana na ya muda mrefu ya kijamii, kiusalama, kisiasa na kiuchumi. Ni ya kisasa kwa kutambua kwamba tuko katikati ya mageuzi makubwa ulimwenguni, na kwamba mabadiliko yanayotokana na hilo katika maisha yetu ya kila siku yanaathiri mazingira ya sasa ambamo uhamiaji unatokea na unajadiliwa.

Kitu gani kimetokea katika uhamiaji?

Mengi yametokea katika uhamiaji katika miaka miwili iliyopita tangu kutolewa kwa *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018* mwishoni mwa mwaka wa 2017.[5] Dunia imeshuhudia **mabadiliko ya kihistoria katika kiwango cha kimataifa** huku Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zikikutana kukamilisha mikataba miwili ya kimataifa juu ya udhihirikaji kimataifa kwa uhamiaji na ufurushwaji: Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji Salama, wenye Utaratibu na Unaokubalika, na Mkataba wa Kimataifa wa Wakimbizi. Kukamilika kwa mikataba hiyo ni matokeo ya juhudi za miongo kadhaa za Mataifa, mashirika ya kimataifa, asasi za kiraia na wahusika wengine

1 Marie McAuliffe, Mkuu, Kitengo cha Utafiti wa Sera ya Uhamiaji, IOM na Binod Khadria, Profesa, Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru.
2 Tazama, kwa mfano, Castles, 2010; Goldin, Cameron na Balarajan, 2011; Koser, 2016; Triandafyllidou, 2018.
3 Ikenberry, 2018; Stone, 2016.
4 Mishra, 2017.
5 IOM, 2017.

(kama mashirika ya sekta binafsi) kuboresha jinsi uhamiaji unasimamiwa katika kiwango cha kimataifa. Katika miaka ya awali kabla tu Mataifa kujitolea kukuza mikataba,[6] mazungumzo, warsha, mashauriano na matukio ya pembeni kadhaa katika viwango vya kimataifa, kikanda, kitaifa na vile vile vya maeneo mahususi vimewezesha "hali halisi" tofauti za uhamiaji kusimuliwa kwa wengine na maeneo mengi ya masilahi ya wengi kupanuliwa kupitia uelewa wa kina wa faida za uhamiaji pamoja na changamoto unazoweza kuleta. Kwa hiyo, mikataba hii, inajengwa kwenye msingi wa miaka mingi ya mashauriano juu ya maswala muhimu yanayounda hoja za mikataba hiyo miwili.

Ukweli unaosikitisha ni kwamba kumekuwepo **matukio makubwa ya uhamiaji na ufurushwaji** katika kipindi cha miaka miwili iliyopita; matukio ambayo yamesababisha dhiki kubwa na kiwewe pamoja na vifo. Kwanza kumekuwepo na ufurushwaji wa mamilioni ya watu kwa sababu ya migogoro (kama vile ndani ya na kutoka Jamhuri ya Kiarabu ya Syria, Yemeni, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Sudan Kusini), vurugu kali (kama zile walizopitia Rohingya hadi wakalazimika kutafuta usalama nchini Bangladeshi) au ukosefu mkubwa wa utulivu wa kiuchumi na kisiasa (kama unaokabili mamilioni ya watu wa Venezuela). Kumekuwepo pia na ongezeko la utambuzi wa athari za mabadiliko ya mazingira na tabianchi kwa mwendo wa binadamu (kama vile uhamiaji uliopangwa/ kuhamishwa hadi kwenye makao mapya na kufurushwa), pamoja na kama sehemu ya juhudi za ulimwengu na mifumo ya sera za kimataifa kushughulikia athari pana za mabadiliko ya tabianchi.[7] Ufurushwaji wa kiwango kikubwa uliosababishwa na hatari zinazohusiana na tabianchi na hali ya hewa ulitokea katika sehemu nyingi za ulimwengu katika miaka ya 2018 na 2019, ikiwa ni pamoja na Msumbiji, Ufilipino, Uchina, Uhindi na Marekani.[8]

Tumeona pia **ongezeko la kiwango cha uhamiaji wa kimataifa kulingana na mienendo ya hivi karibuni**. Idadi ya wahamiaji wa kimataifa inakadiriwa kuwa karibu milioni 272 ulimwenguni, huku karibu theluthi mbili wakiwa wahamiaji wafanyikazi.[9] Idadi hii bado ni asilimia ndogo sana ya idadi ya watu ulimwenguni (ikiwa 3.5%), ikimaanisha kuwa idadi kubwa ya watu ulimwenguni (96.5%) wanakisiwa kuishi katika nchi ambayo walizaliwa. Hata hivyo, idadi inayokadiriwa na kiwango cha wahamiaji wa kimataifa tayari inazidi makadirio yaliyofanywa kuhusu mwaka 2050, ambayo yalikuwa asilimia 2.6 au milioni 230.[10] Licha ya hayo, inatambuliwa kwingi kwamba kiwango na kasi ya uhamiaji wa kimataifa ni ngumu kutabiri kwa usahihi kwa sababu imeunganishwa kwa karibu na matukio mabaya (kama vile ukosefu mkubwa wa utulivu, mzozo au mgogoro wa kiuchumi) pamoja na mienendo ya muda mrefu (kama vile mabadiliko ya idadi ya watu, maendeleo ya kiuchumi, maendeleo ya teknolojia ya mawasiliano na ufikiaji wa usafirishaji).[11] Tunajua pia kutoka kwa data ya muda mrefu kwamba uhamiaji wa kimataifa haufanani ulimwenguni kote lakini unaathiriwa na sababu za kiuchumi, kijiografia, idadi ya watu na sababu zingine zinazosababisha mikondo tofauti ya uhamiaji, kama "njia" za uhamiaji zilizokua kwa miaka mingi (tazama sura ya 3 ya ripoti hii kwa utondoti). Njia kubwa zaidi huwa kutoka nchi zinazoendelea hadi nchi zenye uchumi mkubwa kama zile za Marekani, Ufaransa, Shirikisho la Urusi, Milki za Kiarabu na Saudi Arabia. Kuna uwezekano kwamba ruwaza hii itabaki hivyo kwa miaka mingi ijayo, hasa kwa kuwa idadi ya watu katika baadhi ya sehemu na nchi zinazoendelea inakadiriwa kuwa itaongezeka katika miongo ijayo, na kuweka shinikizo la uhamiaji kwa vizazi vijavyo.[12]

Mambo muhimu kutoka Sehemu ya I ya ripoti kuhusu data na habari kuhusu uhamiaji na wahamiaji yameelezwa kwa muhtasari hapa chini. Habari zaidi na majadiliano yametolewa katika ripoti.

6 Kujitolea kwa mataifa kulielezwa katika Azimio la New York la 2016 la Wakimbizi na Wahamiaji (UNGA, 2016).

7 Tazama sura ya 9 ya ripoti hii kwa majadiliano ya kina.

8 Tazama sura za 2 na 3 za ripoti hii kwa majadiliano kuhusu data na habari za uhamiaji ulimwenguni na katika kanda.

9 UN DESA, 2019a; ILO, 2018.

10 Tazama, kwa mfano, IOM, 2003.

11 WEF, 2019; UN DESA, 2003.

12 UN DESA 2019b.

Mambo muhimu kutoka Sehemu ya I: Data na habari kuhusu uhamiaji na wahamiaji

Idadi ya wahamiaji wa kimataifa ulimwenguni katika mwaka wa 2019: Milioni 272 (3.5% ya idadi ya watu duniani)

- Asilimia 52 ya wahamiaji wa kimataifa walikuwa wanaume; Asilimia 48 walikuwa wanawake.
- Asilimia 74 ya wahamiaji wote wa kimataifa walikuwa na umri wa kufanya kazi (miaka 20-64).

India iliendelea kuwa nchi wanakotoka wahamiaji wengi zaidi wa kimataifa

- India ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya wahamiaji wanaoishi nje ya nchi (milioni 17.5), ikifuatiwa na Meksiko na Uchina (milioni 11.8 na milioni 10.7 mtawalia).
- Marekani iliendelea kuwa nchi iliyovutia wahamiaji wengi ilibaki (wahamiaji milioni 50.7 wa kimataifa).

Idadi ya wahamiaji ilipungua kidogo katika nchi zenye mapato ya juu huku ikiongezeka kwingineko

- Kati ya 2013 na 2017, nchi zenye mapato ya juu zilikumbwa na upungufu mdogo wa wafanyikazi wahamiaji (kutoka milioni 112.3 hadi milioni 111.2). Nchi za mapato ya kati za juu zilipata ongezeko kubwa zaidi (kutoka milioni 17.5 hadi milioni 30.5).
- Kote ulimwenguni, wafanyikazi wahamiaji wa kiume walikuwa wengi kuliko wafanyikazi wahamiaji wanawake kwa milioni 28 katika mwaka wa 2017. Kulikuwa na wafanyikazi wahamiaji wanaume milioni 96 (58%) na wafanyikazi wahamiaji wanawake milioni 68 (42%).

Pesa zinazotumwa kutoka nchi za nje ziliongezeka hadi Dola bilioni 689 za Marekani katika mwaka wa 2018

- Wapokeaji 3 wa juu wa pesa zilizotumwa kutoka nchi za nje walikuwa India (Dola bilioni 78.6 za Marekani), Uchina (Dola bilioni 67.4 za Marekani) na Meksiko (Dola bilioni 35.7 za Marekani).
- Marekani iliendelea kuwa nchi inayotuma pesa nyingi sana hadi nchi za nje (Dola bilioni 68.0 za Marekani) ikifuatiwa na Milki za Kiarabu (Dola bilioni 44.4 za Marekani) na Saudi Arabia (Dola bilioni 36.1 za Marekani).

Idadi ya wakimbizi ulimwenguni ilikuwa milioni 25.9 katika mwaka wa 2018

- Wakimbizi milioni 20.4 walikuwa chini ya mamlaka ya Shirika la Wakimbizi la Umoja wa Mataifa (UNHCR) na milioni 5.5 walikuwa wakimbizi wa Kipalestina chini ya mamlaka ya Shirika la Usaidizi na Kazi la Umoja wa Mataifa kwa Wakimbizi wa Palestina (UNRWA) katika Mashariki ya Karibu.
- Asilimia 52 ya idadi ya wakimbizi ulimwenguni walikuwa chini ya umri wa miaka 18.

Idadi ya wakimbizi wa ndani iliyotokana na vurugu na migogoro ilifikia milioni 41.3

- Hii ndiyo ilikuwa idadi kubwa zaidi iliyorekodiwa tangu Kituo cha Ufuatiliaji wa Wakimbizi wa Ndani kilipoanza ufuatiliaji katika mwaka wa 1998.
- Jamhuri ya Kiarabu ya Syria ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu waliokimbia makazi yao (milioni 6.1) ikifuatiwa na Colombia (milioni 5.8) na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (milioni 3.1).

Idadi ya watu wasio na utaifa ulimwenguni katika mwaka wa 2018 ilikuwa milioni 3.9

- Bangladeshi ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya watu wasio na utaifa (karibu 906,000). Ilifuatiwa na Côte d'Ivoire (692,000) na Myanmar (620,000).

Kwa maelezo zaidi, rejelea sura ya 2 ya ripoti hii. Vyanzo na tarehe za makadirio yaliyo hapo juu vimeelezwa kwa ufupi katika sura hii.

Ruwaza za uhamiaji zinatofautiana kutoka ukanda mmoja hadi mwingine

- Huku wahamiaji wengi wa kimataifa waliozaliwa Afrika, Asia na Ulaya wakiwa wanaishi katika kanda zao za kuzaliwa, wahamiaji wengi kutoka Amerika Kusini na Karibiani na Amerika ya Kaskazini wanakaa nje ya kanda zao za kuzaliwa. Huko Oceania, idadi ya wahamiaji wa ndani ya ukanda na wale wanaoishi nje ya ukanda huo ilibaki sawa katika mwaka wa 2019.
- Zaidi ya nusu ya wahamiaji wa kimataifa (milioni 141) waliishi Ulaya na Amerika Kaskazini.

Uhamiaji umekuwa kiamuzi muhimu cha mabadiliko ya idadi ya watu katika nchi kadhaa

- Uhamiaji wa ndani ya ukanda umekuwa mchangiaji muhimu wa mabadiliko ya idadi ya watu katika baadhi ya nchi za Kiafrika kama Equatorial Guinea.
- Uhamiaji wa wafanyikazi umechangia mabadiliko makubwa ya idadi ya watu hasa katika Mataifa ya Baraza la Ushirikiano wa Ghuba (GCC). Bila kujumuisha Oman na Saudi Arabia, wahamiaji walichangia idadi kubwa ya watu katika nchi za GCC.

Ufurushwaji ulibaki kuwa tukio kuu katika kanda zingine

- Jamhuri ya Kiarabu ya Syria na Uturuki zilikuwa asili na wenyeji wa idadi kubwa zaidi ya wakimbizi ulimwenguni, milioni 6.7 na milioni 3.7, mtawalia. Canada ikawa nchi kubwa zaidi ya makazi mapya ya wakimbizi, ikitoa makazi mapya kwa wakimbizi wengi zaidi kuliko Marekani katika mwaka wa 2018.
- Ufilipino ilikuwa na idadi kubwa zaidi ya ufurushwaji uliotokana na majanga mapya katika mwaka wa 2018 (milioni 3.8).
- Karibu wananchi milioni 4 wa Venezuela walikuwa wameondoka nchini mwao kufikia katikati ya 2019. Jamhuri ya Bolivaria ya Venezuela ilikuwa nchi iliyo chanzo kikubwa cha watafuta hifadhi katika mwaka wa 2018 (zaidi ya 340,000).

Kwa maelezo zaidi, rejelea sura ya 3 ya ripoti hii. Vyanzo na tarehe za makadirio yaliyo hapo juu vimeelezwa kwa ufupi katika sura hii.

Matokeo ya utafiti na uchanganuzi wa uhamiaji yalibaki kuwa ya juu

- Kulikuwa na mfululizo wa ongezeko la idadi ya machapisho ya kitaaluma yanayohusiana na uhamiaji, huku machapisho mengi zaidi ya kitaaluma yakitolewa katika kipindi cha miaka miwili iliyopita. Kulikuwa na mchango mkubwa kutoka kwa mashirika ya kimataifa juu ya maswala anuwai ya uhamiaji.
- Mchango wa kitaaluma kuhusu uhamiaji unatawaliwa na taswira kutoka nchi zinazopokea wahamiaji, hasa kuhusiana na Ulaya. Ulinganishaji wa kijiografia wa ushiriki wa msingi wa waandishi katika majarida yaliyochaguliwa unaonyesha kuwa wengi wanatoka kwenye taasisi zilizo katika nchi zilizoendelea.

Kwa maelezo zaidi, rejelea sura ya 4 ya ripoti hii. Vyanzo na tarehe za makadirio yaliyo hapo juu vimeelezwa kwa ufupi katika sura hii.

Je, uhamiaji unabadilika, au ni usawiri wa uhamiaji unaobadilika?

Kama inavyoonekana kutoka kwa majadiliano na maelezo muhimu hapo juu, kumekuwepo na mabadiliko ya kuongezeka kwa uhamiaji katika miaka ya hivi karibuni, kama vile katika kiwango jumla cha uhamiaji na ufurushwaji, ingawa mabadiliko haya hayangeweza kuelezewa kuwa "ni makubwa". Badala yake, itaonekana kuwa kumekuwepo na uimarikaji wa ruwaza zilizopo za uhamiaji kwani fursa zilizoletwa na ukuaji wa uchumi na mageuzi, uhurishaji wa biashara na utulivu wa muda mrefu zimefanikishwa zaidi. Pia kuna ushahidi unaokua unaoonyesha kwamba huku dhana jumla ya uhamiaji wa kimataifa ikaonekana kuwa rahisi na ya moja kwa moja - kama inavyoonyeshwa katika vyombo vya habari, kwa mfano - uchangamano wake unaendelea kudhihirika zaidi.[13] Suala la jinsi tunavyofikiria juu ya uhamiaji na mwendo limechunguzwa kwa muda mrefu na wasomi na watunga sera wengi.[14] Hivi karibuni, wengine walitaka lifikiriwe upya, wakionyesha shida zinazoongezeka zinazotokana na maoni yasiyobadilika kuhusu "uhamiaji" - tazama sanduku la maandishi lililo hapa chini kuhusu makala ya hivi karibuni ya Profesa Ronald Skeldon juu ya mada hii.

Kufikiria upya kuhusu uhamiaji wa kimataifa, uhamiaji wa ndani ya nchi, mwendo na ukuaji wa miji

Inakubaliwa kuwa uhamiaji ndiyo shida kubwa zaidi kati ya vigezo geu vya idadi ya watu. Tofauti na matukio ya kipekee ya kuzaliwa na kifo ambayo ni matukio muhimu katika maisha ya mtu binafsi, uhamiaji unaweza kutokea mara nyingi. Kipimo chake kinategemea kikamiifu jinsi unavyofafanuliwa kiwakati na katika nafasi.

…

Licha ya shida zote zilizo katika ukusanyaji wa data ya uhamiaji, maendeleo makubwa yamepatikana katika miaka ya hivi karibuni. Mkusanyiko wa hifadhidata ya asili-kikomo cha safari ulimwenguni, ulioundwa mwanzo katika Chuo Kikuu cha Sussex na sasa umepanuliwa sana na kuendelezwa na Kitengo cha Idadi ya Watu cha Umoja wa Mataifa na Benki ya Dunia, umetoa mfumo wa kipimo sahihi zaidi cha mwendo wa idadi ya watu ulimwenguni.a Data hizi zilionyesha kuwa karibu asilimia 3 ya idadi ya watu ulimwenguni waliishi katika Taifa au eneo lisilo walikozaliwa na kwamba kiwango hicho hakikuwa kimebadilika sana tangu miaka ya 1990… Jinsi mifumo ya uhamiaji wa ndani ya nchi na kimataifa inavyokua na kubadilika, ndivyo pia hali ya uhusiano kati yao… aina zingine za uhamaji wa muda mfupi huibuka hasa kutoka kwa tamaduni na uchumi wa mijini.

…

Dhana kwamba watu wengi hawahami au wametuama mahali maalum inaweza kuwa inavutia lakini si sahihi. Uhamaji ni tabia ya asili ya watu wote isipokuwa kama sera maalum au mambo mengine yamewekwa ambayo yanapunguza au kudhibiti uhamaji huo. Hata hivyo, watu wengine wanaonekana kuhama zaidi kuliko wengine na kwa njia tofauti na wengine, jambo ambalo linaonekana kuhusishwa kwa karibu na kiwango cha maendeleo katika kila nchi, hali ambayo, pia, inahusishwa na usambaaji wa watu katika kila nchi. Licha ya shida zote zilizopo katika upimaji wa uhamiaji wa ndani ya nchi kama ilivyoelezwa kwa ufupi hapo juu, maendeleo makubwa yamepatikana katika ujenzi wa modeli za uchambuzi ambazo zinawezesha ulinganishaji wa ruwaza kila mahali.

a Parsons na wengine, 2007; UN DESA, 2015.
Kifupisho cha dondoo la Skeldon, 2018.

13 Czaika na de Haas, 2014; De Witte, 2018; Hall na Posel, 2019.

14 Faist na Glick-Schiller, 2009; Hochschild na Mollenkopf, 2008; King, 2012.

Hata hivyo, lazima tutambue kwamba kuongezeka kwa uchangamano wa uhamiaji ni, kwa kiasi fulani, pia kwa sababu ya kuwepo kwa habari zaidi juu ya uhamiaji na wahamiaji kuliko hapo awali. Tunajua mengi zaidi juu ya nani anayehama, kwa nini watu wanahama, wapi na jinsi wanavyohama, ingawa labda si kwa kiwango ambacho tungependa. Lakini ni wazi kuwa suala kubwa la "uchangamano" linatumika kwa mabadiliko mengi sana yanayotokea ulimwenguni. Baadhi ya yale mahususi, yaliyoangaziwa katika kisanduku cha maandishi kilicho hapa chini, yamechunguzwa sana na kuchambuliwa na wataalam katika Sehemu ya II ya ripoti hii.

Mambo muhimu kutoka Sehemu ya II: Maswala tata na yanayoibuka ya uhamiaji

- Wahamiaji wametoa michango mikubwa ya kijamii, kitamaduni, kisiasa na kiuchumi katika nchi za asili na nchi walizohamia, pamoja na kuwa mawakala muhimu wa mabadiliko katika sekta mbalimbali (sura ya 5).
- Kwa kawaida, wahamiaji huwa na shughuli nyingi za ujasiriamali wakilinganishwa na wenyeji. Katika nchi kama Marekani, wahamiaji wamechangia uvumbuzi kwa kiasi kisicho urari (sura ya 5).
- Ujumuishaji wa wahamiaji katika jamii inayowapokea kunahusiana na maeneo anuwai ya jamii/sera ambazo zinategemeana kwa karibu. Matokeo ya ujumuishaji katika eneo moja la sera - kama vile lugha, elimu, ujumuishaji wa soko la ajira, kuungana tena kwa familia, ushiriki wa kisiasa na kuandikisha uraia - kunaweza kuathiri wengine (sura ya 6).
- Kuna uhusiano mkubwa na ulio changamano kati ya uhamiaji na afya ambao haukujifunga katika migogoro tu. Uhamiaji unaweza kusababisha uwezekano mkubwa wa kuwepo hatari za kiafya lakini pia unaweza kuhusishwa na afya bora, hasa kwa wale wanaotafuta usalama kutokana na madhara (sura ya 7).
- Huku watoto wengi wanaohama hufanya hivyo kupitia michakato salama ya uhamiaji kama sehemu ya kitengo cha familia, watoto wahamiaji wengi wengine hawana ulinzi madhubuti dhidi ya madhara na wanakabiliwa na ukiukaji wa haki za binadamu katika hatua zote za safari zao (sura ya 8).
- Makadirio ya hivi karibuni ya ulimwengu ya idadi jumla ya wahamiaji watoto ni takriban milioni 31. Kuna takriban wakimbizi watoto milioni 13, watoto 936,000 wanaotafuta hifadhi, na watoto milioni 17 ambao wamehamishwa kwa nguvu ndani ya nchi zao (sura ya 8).
- Kuna ushahidi unaoongezeka kwamba ukubwa na idadi ya marudio ya hali ya hewa iliyokithiri vinaongezeka, na hii inatarajiwa kuzidi kuathiri uhamiaji na aina zingine za mwendo. Huku uhamaji wa binadamu unaotokana na mabadiliko ya mazingira na tabianchi mara nyingi huelezwa kwa misingi ya ulinzi na usalama, kuelewa uhamaji kama urekebishaji ili kuendana na hali mpya huruhusu wakala wa wahamiaji kuwa sehemu ya wanaojitokeza kutoa suluhu (sura ya 9).
- Hali ya uhamiaji inaweza kuathiri sana uwezo wa wahamiaji kushughulikia migogoro. Sera nyumbushi za uhamiaji na viza husaidia kuwawezesha wahamiaji kujiweka salama na vilevile kupata nafuu kutokana na athari za mgogoro. Kurejea ni njia moja, lakini si mwitiko ulio chaguo la kimsingi (sura ya 10).

- Miaka miwili iliyopita kumetokea mabadiliko makubwa katika utawala wa kimataifa wa uhamiaji, hasa katika uundaji wa Mtandao wa Uhamiaji wa Umoja wa Mataifa na mikataba miwili ya ulimwengu juu ya wakimbizi na uhamiaji. Ingawa haimfungi mtu kisheria, mikataba hii miwili ya ulimwengu inawakilisha makubaliano yaliyofikiwa karibu kote ulimwenguni juu ya maswala yanayohitaji ushirikiano endelevu wa kimataifa na kujitolea (sura ya 11).

Kasi ya mabadiliko ambayo haijawahi kutokea katika nyanja za kisiasa (zinazoathiriwa na masuala ya kijiografia), kijamii, kimazingira na kiteknolojia imesababisha baadhi ya wachambuzi na wafafanuzi kubuni au kutumia misemo kama "kipindi cha mchapuko",[15] "mapinduzi ya nne ya viwanda",[16] na " kipindi cha mabadiliko ".[17] Kuna utambuzi mpana wa jinsi ulimwengu unavyobadilika haraka, na jinsi kasi ya mabadiliko inavyoonekana kuchapuka kuzidi matarajio na utabiri wote. Pia kuna namna ambayo mabadiliko yanasababisha athari zisizotarajiwa (na zisizohitajika):

> Tunaishi katika enzi ya msukosuko, kukata tamaa na mkanganyiko mkali. Mivutano inayoongezeka ya siasa za kijiografia inabadilisha uhusiano wa kimataifa, na siasa za kikabila zinadhihirisha migawanyiko mikubwa ndani ya nchi mbalimbali. Uenezi wa teknolojia zinazoharakisha utendaji unabadilisha mawazo ya muda mrefu kuhusu usalama, siasa, uchumi na mengine mengi.[18]

Cha kuzingatia zaidi ni mabadiliko makubwa yaliyotokea katika eneo la kisiasa, hasa katika suala la kushirikisha raia kupitia mitandao ya kijamii inayoibuka na majukwaa mengine ya mtandaoni pamoja na viwango vya uongozi wa kisiasa. "Vuguvugu la Uarabuni", kwa mfano, lilianzisha maendeleo muhimu ya jinsi sauti za umma zilivyosikilizwa na wanaharakati wakapangwa katika medani za kisiasa.[19] Hivi karibuni, tumeona ongezeko kubwa la uchambuzi na utoaji maoni juu ya mabadiliko ambayo yanatokea katika mifumo ya kidemokrasia kote ulimwenguni, na athari zake kwa utawala, siasa za kijiografia na ushirikiano wa kimataifa. Tunaishi katika kipindi ambacho maadili ya msingi yanayoimarisha uongozi ulimwenguni yanapingwa. Maadili ya usawa, uwajibikaji, kutopendelea, haki na uadilifu yanadhoofishwa sana wakati viongozi wengine wa kisiasa wanapuuza masilahi ya wengi kwa kuhiari masilahi ya kibinafsi - hata ikiwa yanakiuka sheria, michakato na taasisi ambazo, kwa jumla, zilijaribu kuendeleza mataifa mazima na watu, bila kuwatenga au kuwafukuza wengine kwa sababu ya sifa zao za asili au imani.[20] Ukiukaji wa kimfumo na unaoendelea, kama ulivyoshuhudiwa katika historia, unaweza kuenea hadi kwa mashambulizi dhidi ya haki za binadamu na mwishowe kwa vikundi vya watu katika jamii.[21]

Kama sehemu ya mabadiliko ya sasa, uhamiaji wa kimataifa umezidi kufanywa silaha. Unatumiwa na wengine kama zana ya kisiasa, kuhujumu demokrasia na ushirikishwaji wa raia, kwa kutumia hofu inayofahamika katika jamii mbalimbali ambayo inatokana na kasi iliyozidishwa ya mabadiliko na ongezeko la mashaka ya nyakati zetu.[22] Viongozi wengine wanajaribu kugawanya jamii mbalimbali kuhusu suala la uhamiaji,

15 Friedman, 2016.
16 Schwab, 2016.
17 Mauldin, 2018.
18 Muggah na Goldin, 2019.
19 AlSayyad na Guvenc, 2015.
20 Fotaki, 2014.
21 Rawnsley, 2018.
22 Ritholtz, 2017.

wakidharau faida kubwa na utajiri ambao uhamiaji huleta na kupuuza bila kusita historia zetu za uhamiaji. Na tunazidi kushuhudia utumiaji wa mitandao ya kijamii kama njia ya kugawanya na kutenga, si tu kwa uhamiaji, lakini wakati fulani tumeona wanaharakati wakitumia "mbinu za kikabila" mtandaoni wakijaribu kusawiri uhamiaji kwa njia hasi na ya kupotosha[23] Linaloimarisha usawiri huu unaobadilika wa uhamiaji wa kimataifa ni matumizi ya uvumbuzi wa teknolojia, hasa teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT). Hata hivyo, lazima pia tukumbuke kwamba siasa ya uhamiaji si mpya, kama inavyosisitizwa katika sanduku la maandishi hapa chini.

Suala la kudumu la siasa: Dondoo kutoka *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2003*[a]

Uhamiaji ni mada maarufu ya kisiasa. Katika mwongo mmoja uliopita, siasa za uhamiaji zimedhihirishwa na mfuatano wa matukio: hofu katika nchi za Magharibi ya kuongezeka kwa umati wa wahamiaji kutoka nchi za Muungano wa Urusi wa zamani na katika nchi za Umoja wa Ulaya kuhusu uvamizi wa raia kutoka kwa nchi wanachama wapya kila wakati Umoja unapopanuliwa; kuhoji kuhusu wajibu wa wahamiaji katika misukosuko ya kiuchumi na kijamii iliyosababishwa na migogoro ya kifedha huko Kusini-Mashariki mwa Asia; sera zisizo huru na upinzani dhidi ya uhamiaji baada ya mashambulio ya kigaidi ya Septemba 11, 2001; kuzuka upya kwa mlipuko wa chuki dhidi ya wageni katika nchi kadhaa za Kiafrika ambazo zinalaumu wahamiaji kwa mizozo ya ndani ya nchi; na baadhi ya wanasiasa kutumia masuala ya uhamiaji ili kupata manufaa katika uchaguzi. Mifano hii yote inaonyesha uhusiano wa karibu kati ya masuala ya kiuchumi, kisiasa na kijamii kwa upande mmoja, na uhamaji kwa upande mwingine. Kwa hivyo, zaidi ya wakati wowote, uhamiaji ni kisingizio cha mashambulizi chenye vidokezo vya kisaikolojia, kiuchumi, na uhusiano wa umma.

a IOM, 2003.

Teknolojia kama kiwezeshaji na kibadilisha mambo

Uhamiaji umeunganishwa na teknolojia na uvumbuzi na kuna kusanyiko kubwa la uchambuzi ambalo limekadiria jinsi uhamiaji wa kimataifa unavyofanya kazi kusaidia (na wakati mwingine kupunguza) uhamishaji wa teknolojia na maarifa, mara nyingi ukifanya kazi kwa ushirikiano na uwekezaji na mtiririko wa biashara katika uhusiano wa kihistoria, kijiografia na wa siasa za kijiografia kati ya nchi na jamii.[24] Teknolojia inazidi kuwa muhimu wakati wote wa mchakato wa uhamiaji, hasa aina mpya za teknolojia. Katika miaka ya hivi karibuni, kwa mfano, tumeshuhudia wahamiaji wakitumia TEHAMA kukusanya habari na ushauri kwa wakati halisi wakiwa katika safari za uhamiaji; suala ambalo linawavutia watu na, wakati mwingine, kutia wasiwasi. Matumizi ya TEHAMA, kama vile programu za kushiriki habari za hivi punde, pamoja na kusaidia kuvuka mipaka kwa siri, na pia ujumuishaji wa majukwaa ya mitandao ya kijamii kuunganisha vikundi vilivyotawanyika kijiografia vyenye masilahi yanayofanana, yameibua maswali halali kuhusu kiwango ambacho teknolojia imetumika kusaidia uhamiaji usiofuata kanuni, na pia kuwezesha wahamiaji kuepuka wafanya magendo ya wahamiaji na wanaofanya biashara haramu ya kusafirisha binadamu walio

23 McAuliffe, 2018.

24 Burns na Mohapatra, 2008; Kapur, 2001; Khadria, 2004.

dhalimu na wanyonyaji.[25] Kwa sababu ya kuongezeka kwa ufikiaji wa teknolojia inayoibuka kwa gharama ya chini, wahamiaji pia wameunda programu za kusaidia ujumuishaji bora katika nchi zinazowapokea, huku wanadumisha viungo vya kijamii na msaada wa kifedha kwa familia na jamii zao zilizo nyumbani, pamoja na kupitia kwa programu za "pesa za rununu" zinazoongezeka na kuenea.

Miungano mingine kati ya uhamiaji na teknolojia pia inaibuka katika mijadala ya uhamiaji. Jinsi akili ya bandia inavyokubaliwa hatua kwa hatua katika sekta muhimu, matokeo yake kwa mtiririko wa wafanyikazi wahamiaji na masoko ya wafanyikazi wa ndani ni maeneo ya kuzingatiwa sana na watunga sera na biashara katika nchi asili na zinazopokea wahamiaji.[26]

Majadiliano ya hivi karibuni pia yamegeukia teknolojia ya *blockchain* na matokeo yake kwa uhamiaji, hasa kwa pesa zinazotumwa kutoka nchi za nje, lakini pia kwa utambulisho wa kidijitali na uhamaji ulimwenguni.[27] Teknolojia ya mitandao ya kijamii pia inazidi kuathiri siasa za uhamiaji, kukiwa na ongezeko la uhamasishaji wa mrengo wa kulia kwenye majukwaa ya mitandao ya kijamii yanayojaribu kushawishi mijadala ya kisiasa na mwishowe maamuzi ya kisiasa.[28]

Ni katika muktadha huu wa sasa wa mabadiliko makubwa na ongezeko la mashaka ambapo *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2020* inajaribu kutumia kusanyiko la data, utafiti na uchambuzi uliopo ili kuchangia uelewa tofauti zaidi wa baadhi ya masuala muhimu zaidi na ya dharura ya wakati wetu kuhusu uhamiaji duniani. Kutokana na asili yake, mienendo changamano ya uhamiaji haiwezi kupimwa, kueleweka na kudhibitiwa kikamilifu. Hata hivyo, kama ripoti hii inavyoonyesha, tunalo kusanyiko la data na habari linaloendelea kukua na kuwa zuri zaidi ambalo linaweza kutusaidia kuelewa vyema sifa za msingi za uhamiaji na namna zinavyobadilika - pamoja na kuelewa namna muktadha ambamo uhamiaji unatokea unavyobadilika. Hili linazidi kuwa muhimu kwani mijadala ya umma, iliyojaa habari potofu na za uwongo, inazidi kuwa na uwezo wa kutumia upanuzi unaoendelea wa majukwaa wazi ya "vyombo vipya vya mawasiliano" kufikia upotoshaji na uwasilishaji visivyo wa uhamiaji na wahamiaji.

Mfululizo wa Ripoti za Uhamiaji Duniani

Ripoti ya kwanza ya Uhamiaji Duniani ilichapishwa miaka 20 iliyopita, hapo awali ilichapishwa kama ripoti ya mara moja tu iliyokusudiwa kuongeza uelewa wa watunga sera na umma kwa jumla kuhusu uhamiaji. Ilibuniwa wakati ambapo athari za utandawazi zilikuwa zikihisika katika sehemu nyingi za dunia na kwa njia nyingi. Kwa kweli, Ripoti ya kwanza ya Uhamiaji Duniani inataja kwamba sehemu ya asili yake ilitokana na athari za utandawazi kuhusu ruwaza za uhamiaji, na kwamba ripoti hiyo kwa hivyo "inaangalia uchumi wa ulimwengu unaokua ambao umesababisha wingi wa wageni usiowahi kutokea katika nchi nyingi…" .[29] Ripoti hiyo iliangazia ukweli kwamba, licha ya kuwa "tukio la zamani", uhamiaji ulikuwa unachapua kama sehemu ya mabadiliko makubwa ya utandawazi wa michakato ya uchumi na biashara, ambayo ilikuwa ikiwezesha mwendo mkubwa za wafanyikazi na vilevile bidhaa na mitaji. Jedwali la 1 hapa chini linatoa muhtasari wa

25 McAuliffe, 2016; Sanchez, 2018.

26 McAuliffe, 2018.

27 Latonero et al., 2019; Juskalian, 2018.

28 Tazama sura ya 5 ya ripoti hii kwa majadiliano ya jinsi majukwaa ya mitandao ya kijamii yanavyobadilisha mijadala ya umma kuhusu uhamiaji.

29 IOM, 2000.

takwimu muhimu zilizoripotiwa katika *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2000*, ikilinganishwa na toleo hili la sasa. Inaonyesha kuwa ingawa mambo kadhaa hayajabadilika - kiwango cha wahamiaji wa kimataifa wanawake na pia kiwango jumla cha idadi ya watu ulimwenguni ambao walikuwa wahamiaji - mambo mengine yamebadilika sana. Kwa mfano, utumaji pesa kimataifa umekua kutoka wastani wa bilioni 126 katika mwaka wa 2000 hadi bilioni 689 katika mwaka wa 2020, ukisisitiza umuhimu wa uhamiaji wa kimataifa kama kiendesha maendeleo. Hili linasaidia kueleza kwa kiasi kuibuka kwa uhamiaji kama suala la kiwango cha kwanza ulimwenguni ambalo limeshuhudia Nchi Wanachama wa Umoja wa Mataifa zikichukua hatua kadhaa za kuimarisha udhibiti wa kimataifa wa uhamiaji, hasa tangu mwaka 2000 (angalia sura ya 11 ya ripoti hii kwa majadiliano). Haishangazi basi kwamba Shirika la Kimataifa la Uhamiaji (IOM) lenyewe limekua kwa ukubwa, kukiwa na ongezeko kubwa la wanachama katika miongo miwili iliyopita kutoka 76 hadi wanachama wake wa sasa wa Mataifa 173. Pia, la muhimu katika jedwali la 1 ni ongezeko la wahamiaji wa kimataifa ulimwenguni (karibu 85%) na vilevile wakimbizi (karibu 80%) na wakimbizi wa ndani (hadi karibu 97%); wakati wote huo wakibaki kuwa kiwango kidogo sana cha idadi ya watu ulimwenguni.

Jedwali la 1. Taarifa za ukweli na takwimu muhimu kutoka Ripoti za Uhamiaji Duniani, 2000 na 2020

	Ripoti ya 2000	Ripoti ya 2000
Idadi inayokadiriwa ya wahamiaji wa kimataifa	Milioni 150	Milioni 272
Kiwango kinachokadiriwa cha idadi ya watu ulimwenguni ambao ni wahamiaji	2.8%	3.5%
Kiwango kinachokadiriwa cha wahamiaji wa kimataifa wanawake	47.5%	47.9%
Kiwango kinachokadiriwa cha wahamiaji wa kimataifa ambao ni watoto	16.0%	13.9%
Ukanda wenye kiwango kikubwa zaidi cha wahamiaji wa kimataifa	Oceania	Oceania
Nchi yenye kiwango kikubwa zaidi cha wahamiaji wa kimataifa	Milki za Kiarabu	Milki za Kiarabu
Idadi ya wahamiaji wafanyikazi	-	Milioni 164
Utumaji pesa wa kimataifa ulimwenguni (USD)	Bilioni 126	Bilioni 689
Idadi ya wakimbizi	Milioni 14	Milioni 25.9
Idadi ya wakimbizi wa ndani	Milioni 21	Milioni 41.3
Idadi ya watu wasio na utaifa	-	Milioni 3.9
Idadi ya Nchi Wanachama wa IOM*	76	173
Idadi ya ofisi za nyanjani za IOM*	120	436+

Vyanzo: Tazama IOM, 2000 na toleo la sasa la ripoti hiyo kwa vyanzo.

Maelezo: Tarehe za makadirio ya data kwenye jedwali zinaweza kuwa tofauti na tarehe ya kuchapishwa kwa ripoti (rejelea ripoti hizo kwa utondoti zaidi juu ya tarehe za makadirio); rejelea sura ya 3 ya ripoti hii kwa uainishaji wa kikanda; * inaonyesha kuwa data haikujumuishwa kwenye ripoti lakini ni ya mwaka huo; + kama ilivyokuwa tarehe 28 Oktoba 2019.

Mchango wa *Ripoti ya Uhamiaji ya Dunia 2000* kwa sera ya uhamiaji pamoja na masomo ya uhamiaji ulikuja wakati unaofaa, na mafanikio yake yalianzisha mfululizo wa Ripoti ya Uhamiaji Duniani. Tangu mwaka wa 2000, ripoti kumi za uhamiaji ulimwenguni zimetolewa na IOM (tazama sanduku la maandishi hapa chini) na huu umekuwa mfululizo wa chapisho kuu la shirika. Kinachoendelea kuzingatiwa sana ni kutoa mchango unaofaa, thabiti na unaohimiliwa na ushahidi ambao unaongeza uelewa wa watunga sera, wataalamu, watafiti na umma kwa jumla kuhusu uhamiaji.

Mwishoni mwa mwaka wa 2016, IOM ilifanya uamuzi wa kuboresha mfululizo wa Ripoti ya Uhamiaji Duniani ili kuhakikisha kuwa inaweza kuongeza mchango wake kwa maarifa yaliyojikita kwenye ukweli kuhusu uhamiaji ulimwenguni. Kila toleo la mfululizo huu sasa lina sehemu mbili zinazojumuisha:

- Sehemu ya I: Maelezo muhimu kuhusu uhamiaji na wahamiaji (pamoja na takwimu zinazohusiana na uhamiaji);
- Sehemu ya II: Uchambuzi unaohimiliwa na ushahidi na unaoangalia pande zote za masuala changamano na yanayoibuka ya uhamiaji.

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2000

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2003: Kusimamia Uhamiaji - Changamoto na Mwitikio wa Watu walio kwenye Mwendo

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2005: Gharama na Faida za Uhamiaji wa Kimataifa

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2008: Kusimamia Uhamaji wa Wafanyikazi katika Uchumi wa Ulimwengu Unaobadilika

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2010: Mustakabali wa Uhamiaji: Kujenga Uwezo wa Mabadiliko

Ripoti ya Uhamaji Duniani 2011: Kuwasiliana Kikamilifu kuhusu Uhamiaji

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2013: Ustawi na Maendeleo ya Wahamiaji

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2015: Wahamiaji na Miji: Ushirikiano Mpya wa Kusimamia Uhamaji

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2020

Kuondoka kutoka kwa matoleo ya dhamira moja ya mfululizo wa ripoti hizi hadi kwa muundo huu wa sehemu mbili kulikuwa kwa kutambua mabadiliko makubwa katika utafiti, uchambuzi na uchapishaji wa uhamiaji, na vilevile matarajio na mahitaji tofauti ya wasomaji. Kwa wale ambao wanataka kufahamu taarifa za kweli na takwimu muhimu za uhamiaji, Sehemu ya I imekusanya habari na takwimu za hivi punde ili wasomaji waweze kuelewa vyema mienendo ya uhamiaji, mikondo inayoobadilika na michakato katika viwango vya ulimwengu na kikanda. Lakini kwa wale ambao huenda wanafanyia kazi (au kuchunguza) maeneo mahususi ya sera au utendaji wa uhamiaji, maelezo ya kina kuhusu uchangamano huo yametolewa katika Sehemu ya II. Uboreshaji wa mfululizo huo pia ulikuwa kwa kutambua kwamba, kadiri uzingatiaji wa, na uchangamano wa uhamiaji

unavyozidi kuongezeka, ripoti zilizo na dhamira moja zinaweza kushindwa kueleza kikamilifu au kukosa kabisa mabadiliko mapana ambayo yanatokea katika mageuzi ya uhamiaji ulimwenguni.

Ufikiriaji zaidi wa mfululizo uliorekebishwa ulikuwa ndio "kiongeza-thamani" kilichokusudiwa. Kama shirika la serikali mbalimbali, na shirika jipya linalohusiana na Umoja wa Mataifa, ni muhimu IOM ihakikishe kwamba Ripoti ya Uhamiaji Duniani inahudumia umma katika kutoa habari na uchambuzi unaofaa, unaoweza kufikiwa, thabiti, sahihi na unaozingatia pande zote. Hitaji la kuzuia kurudia au kuingiliana kwa kiasi kikubwa ni la kweli, hasa kwa kwa mujibu wa michango mipya juu ya utawala wa uhamiaji (kama vile Viashiria vya Utawala wa Uhamiaji). Kwa njia hii, mfululizo wa Ripoti ya Uhamiaji Duniani iliundwa upya ili kutoa uchambuzi wa kimkakati wa masuala changamano na yanayoibuka yanayowakabili watunga sera, badala ya kueleza au kutathmini sera na uongozi wa sasa juu ya uhamiaji. Mfululizo huu unajaliza badala ya kurudia kazi nyingine.

Ushahidi unaonyesha kuwa mifululizo iliyorekebishwa imefanikiwa katika kufikia malengo yaliyokusudiwa, kukiwa na majibu chanya kutoka kwa wasomaji, pamoja na Nchi Wanachama, wasomi wahamiaji na wasomaji wa kawaida. Kiashiria kingine kinachotia moyo ni ongezeko kubwa, endelevu la upakuaji katika mwaka wa 2018 na (hadi leo) 2019 wa *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018* kushinda matoleo ya hapo awali.[30]

Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2020

Toleo hili, linalotangaza kumbukumbu ya miaka ishirini ya mfululizo wa Ripoti ya Uhamiaji Duniani, linapata msingi wake katika ripoti ya awali, toleo la 2018, kwa kutoa takwimu zilizosasishwa za uhamiaji katika viwango vya ulimwengu na kanda na pia uchambuzi wa kimaelezo wa masuala changamano ya uhamiaji.

Sehemu ya I, kuhusu "data na habari muhimu juu ya uhamiaji na wahamiaji", inajumuisha sura tofauti kuhusu mienendo na mikondo ya uhamiaji; upekee na maendeleo ya kikanda; na majadiliano ya michango ya hivi karibuni kwa utafiti na uchambuzi wa uhamiaji uliofanywa na wasomi na mashirika mengi tofauti, pamoja na IOM. Sura hizi tatu zimetayarishwa na taasisi ya IOM, ikitegemea kimsingi uchambuzi wa wataalamu wa IOM, weledi wa taaluma na maafisa ulimwenguni kote kulingana na data kutoka kwa mashirika mengi husika. Sura hizo saba katika Sehemu ya II zimeandikwa na watafiti tumizi na watafiti wa kitaaluma wanaochunguza uhamiaji. Zinashughulikia uanuwai wa "masuala changamano na yanayoibuka ya uhamiaji" yanayojumuisha:

- michango ya wahamiaji kwa jamii;
- uhamiaji, ujumuishaji na mshikamano wa kijamii;
- uhamiaji na afya;
- watoto na uhamiaji usio salama;
- uhamiaji na ugeuzaji ili kuendana na mabadiliko ya mazingira;
- wahamiaji waliokabiliwa na mizozo; na
- maendeleo ya hivi karibuni katika utawala wa uhamiaji ulimwenguni.

Huku uchaguzi wa mada hizi ukiwa wa kiuteuzi na kimapendeleo, sura zote katika Sehemu ya II ya ripoti hii zinahusiana moja kwa moja na baadhi ya mijadala mashuhuri na muhimu kuhusu uhamiaji katika ulimwengu wa leo. Mada nyingi kati ya hizi zinapatikana katika kitovu cha mafumbo ambayo watunga sera hukabiliwa

30 Kielelezo cha 6 katika sura ya 4 ya ripoti hii kinatoa takwimu za upakuzi wa Ripoti za Uhamiaji Duniani za miaka ya 2018 na 2015.

nayo wakati wanapojaribu kuunda majibu yanayofaa, yanayowiana na yanayojenga masuala changamano ya sera ya umma yanayohusiana na uhamiaji. Kwa hivyo, sura hizo zinalenga kuongoza mashauriano na majadiliano ya sera ya sasa na ya baadaye kwa kutambua kwa uwazi masuala muhimu, maelezo ya jumla muhimu ya utafiti na uchambuzi unaofaa, na majadiliano ya athari kwa ajili ya utafiti na utengenezaji wa sera wa siku zijazo. Sura hizi hazikusudiwi kuwa za kuelekeza, kwa maana ya kutetea "suluhisho" fulani za sera - hasa kwa sababu muktadha wa karibu ni kiamuzi muhimu cha mipangilio ya sera - lakini inayoarifu na inayofaa kwa kile ambacho kinaweza kuwa mijadala mikali sana.

Sehemu ya I

Sura hii inatoa maelezo ya kijumla ya data na mienendo ya ulimwengu mzima kuhusu wahamiaji wa kimataifa na uhamiaji wa kimataifa (mtiririko). Pia inatoa majadiliano kuhusu vikundi maalum vya wahamiaji - yaani, wafanyikazi wahamiaji, wakimbizi, wanaoomba hifadhi, wakimbizi wa ndani na watu wasio na utaifa - pamoja na pesa zinazotumwa kimataifa. Zaidi ya hayo, sura hii inarejelea kusanyiko lililopo la data za kiprogramu za IOM, hasa juu ya wahamiaji waliopotea, usaidizi wa kurejea nyumbani kwa hiari na kujumuishwa tena katika jamii, utoaji wa makazi mapya, ufuatiliaji wa waliofurushwa na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu. Ingawa data hizi kwa ujumla si za ulimwengu wote au kiwakilishi chake, zinaweza kutoa vidokezo kuhusu mabadiliko ambayo yametokea katika programu na shughuli za IOM ulimwenguni.

Kufuatia maelezo jumla ya kiulimwengu, sura ya 3 inatoa majadiliano ya vipimo muhimu vya, na maendeleo katika, uhamiaji. Mjadala huo unazingatia kanda sita za ulimwengu kama zilivyotambuliwa na Idara ya Umoja wa Mataifa ya Uchumi na Masuala ya Jamii: Afrika, Asia, Ulaya, Amerika ya Kusini na Karibiani, Kaskazini mwa Amerika, na Oceania. Kwa kila moja ya kanda hizi, uchambuzi unajumuisha: i) maelezo jumla na majadiliano mafupi ya takwimu muhimu zinazohusiana na idadi ya watu; na ii) maelezo mafupi ya "sifa muhimu na maendeleo" katika uhamiaji katika kanda, kulingana na data, habari na uchambuzi anuwai, pamoja na kutoka kwa mashirika ya kimataifa, watafiti na wachambuzi. Ili kushughulikia utofauti wa mikondo ya uhamiaji, mienendo na masuala katika kila mojawapo ya kanda sita, masimulizi ya kimaelezo ya "sifa muhimu na maendeleo ya hivi karibuni" huwasilishwa katika kiwango cha ukanda mdogo.

Kuna kiasi kikubwa cha utafiti na uchambuzi juu ya uhamiaji ambao unafanywa na kuchapishwa na wahusika anuwai kama wasomi, serikali, mashirika ya serikali na vikundi vya washauri mabingwa. Sura ya 4 inatoa maelezo jumla teule ya michango kama hiyo, ikisasisha sura juu ya mada kama ilivyotokea kwa mara ya kwanza katika *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018*. Haya maelezo jumla yanazingatia matokeo ya utafiti wa uhamiaji yaliyochapishwa na wasomi na mashirika ya serikali mbalimbali katika mwaka wa 2017 na 2018, ambayo yalishuhudia mchango wa kiwango cha juu kutoka kwa mashirika ya serikali mbalimbali, baadhi yakiwa yalitolewa ili kuarifu Mataifa na wahusika wengine wakati wa majadiliano juu ya Mkataba wa Kimataifa wa Uhamiaji (angalia sura 11 ya ripoti hii kwa majadiliano ya michakato na matokeo ya mkataba).

Sehemu ya II

Sura inayoongoza katika Sehemu ya II inachunguza michango ya kihistoria na ya kisasa ya wahamiaji kwa jamii zinazowapokea na vilevile wale waliorejea mahali pao pa asili. Kwa mtazamo huu, inazingatia maeneo matatu ya msingi ya michango ya wahamiaji: kijamii na kitamaduni, kiraia na kisiasa, na kiuchumi. Aghalabu panapotokea majadiliano yenye mwelekeo hasi kuhusu uhamiaji na wahamiaji, mtu anaweza kukosa kuona

ukweli kwamba wahamiaji wametoa michango mikubwa kwa njia nyingi. Sura ya 5 ya "hali halisi" inaangazia mada ambayo mara nyingi hupuuzwa lakini ni muhimu, ikiweka uchambuzi katika muktadha wa vizuizi vinavyoibuka vya utambuzi wa michango ya wahamiaji ulimwenguni. Sura hiyo inahitimisha kwa kutoa maana yake kwa ajili ya mazungumzo ya sera na kwa utafiti zaidi.

Sura ya 6 inakagua kwa kina suala la kujumuishwa kwa wahamiaji katika jamii zinazowakaribisha ambapo wanajizoesha tamaduni, mila, maadili ya kijamii na lugha mpya. Sura hiyo inatoa maelezo jumla ya maendeleo ya kihistoria ya mitazamo ya sera na istilahi zinazohusiana na mada. Inazungumzia majukumu ya wadau mbalimbali katika kufanikisha ujumuishaji wa wahamiaji, pamoja na umuhimu wa uwekaji wa sera ambayo inahusiana moja kwa moja na kwa njia isiyo ya moja kwa moja na ujumuishaji. Sura hiyo inahitimishwa na majadiliano juu ya maana yake kwa mwitiko wa sera.

Afya na uhamiaji mara nyingi hufikiriwa tu wakati kuna shida, lakini kuna mengi zaidi yanayounganisha hayo mawili. Sura ya 7 inatoa uchambuzi wa maelezo jumla ya maswala muhimu yanayohusiana na afya na uhamiaji, pamoja na faida, udhaifu na uthabiti. Kisha sura hiyo inachunguza majibu ya mifumo ya afya na mitazamo iliyopo, na vilevile upungufu uliopo katika utawala wa uhamiaji na afya. Mafundisho kutoka kwa miongozo ya utendaji bora na ajenda za ulimwengu katika uhamiaji na afya inatolewa.

Sura ya 8 inashughulikia uhamiaji wa watoto ambao haufanani na ruwaza ya jadi ya mtoto mhamiaji anayeandamana au anayefuata familia katika mazingira salama, lakini kwa kiasi ni uhamiaji ambao si salama, kwa mfano, unaotokea kupitia njia zisizofuata kanuni bila familia. Kufuatia njia ya kimaelezo, sura hiyo inafafanua aina tofauti za uhamiaji wa watoto, viendeshaji vyao, na masuala yanayohusiana na data juu ya uhamiaji wa watoto. Inajadili changamoto muhimu za ulinzi zinazoathiri wahamiaji watoto na kushughulikia masuala ya sasa na sera zinazokua za kuyashughulikia. Sura hiyo inachunguza changamoto kuu zinazoibuka na zinazowakabili wahamiaji watoto na inahitimisha kwa kutafakari juu ya vipaumbele vya sera na utafiti.

Ikitoa maelezo jumla ya mwendo wa binadamu na marekebisho ya kukabiliana na mabadiliko ya mazingira na tabianchi, sura ya 9 inachunguza utafiti jarabati kutoka ulimwenguni kote. Mifano anuwai ya tabia inayoweza kubadilika imewasilishwa kutoka maeneo tofauti ya ekolojia hasa yaliyo katika hatari chini ya mabadiliko ya tabianchi, ambayo ni, milima, maeneo yenye ukame na maeneo ya pwani, na pia miji. Mifano hiyo inaangazia mikakati anuwai ambayo inakuza aina moja au kadhaa za uhamiaji. Sura hiyo pia inatoa muhtasari wa mifumo ya sera za kimataifa kuhusu miitikio ya vipengele vya mwendo wa mabadiliko ya mazingira na tabianchi. Sura hiyo inahitimisha na mapendekezo lengwa ya utafiti, sera na utendaji.

Sura ya 10 inazungumzia shida ambazo wahamiaji wamepata. Ikiwasilisha mifano ya shida kama mafuriko, vimbunga, migogoro, na shida ya kisiasa na kiuchumi, inachunguza msaada wa dharura wa sasa na mwitiko wa haraka wa ulinzi. Sura hiyo inatoa maelezo jumla ya miitiko ya eneo mahususi, kitaifa na kimataifa kwa mahitaji kama hayo yanayokabiliwa na aina tofauti za wahamiaji na ufanisi wake. Kwa kuzingatia Mpango wa Wahamiaji katika Nchi zenye Mgogoro, inachunguza miktadha tofauti, miitiko, upungufu, na mafunzo yaliyopatikana katika utayari wa kukabili migogoro na kupata nafuu baada ya kipindi cha mgogoro. Sura hiyo inatoa maelezo jumla ya data zilizopo juu ya wahamiaji wanaokabiliwa na hatari na hali za mazingira magumu katika nchi nyingi na kukadiria upungufu uliopo. Inahitimisha kwa maana za sera na utendaji wa miitiko.

Kama anwani inavyoeleza, sura ya 11 inatoa sasisho juu ya sura ya usimamizi wa uhamiaji katika *Ripoti ya Uhamiaji Duniani 2018*, ikinasa maendeleo muhimu katika usimamizi wa uhamiaji ulimwenguni katika miaka miwili tangu ripoti ya mwisho. Sura hiyo inatoa uchambuzi wa kimaelezo juu ya ukuzaji na kupitishwa kwa mikataba miwili ya ulimwengu, uchambuzi mfupi wa yaliyomo na maeneo ya muungano na muachano,

tathmini ya jinsi inavyoathiri mfumo wa utawala wa uhamiaji ulimwenguni, athari za baadaye pamoja na changamoto kwa utekelezaji. Sura hiyo inazungumzia ahadi za Mataifa kutekeleza na kukagua ufuatiliaji na maendeleo ya mkataba, na inafupisha mabadiliko katika mifumo ya kitaasisi ili kusaidia Mkataba wa Uhamiaji Ulimwenguni. Sura hiyo pia inazingatia masuala ya muda mrefu na maana yake kwa siku zijazo.

Kwa ujumla, ripoti hii ya uhamiaji duniani imetolewa ili kusaidia kukuza uelewa wetu wa pamoja wa udhihirikaji mbalimbali na uchangamano wa uhamiaji wakati huu wa mashaka yanayoongezeka. Tunatumai kwamba wasomaji wote wanaweza kujifunza kitu kipya kutoka kwa toleo hili, na pia kujifunza kutoka kwa yaliyomo wanapofanya kazi zao, wanaposoma au wanapofanya shughuli zingine.

Marejeleo*

AlSayyad, N. na M. Guvenc
2015 Virtual uprisings: On the interaction of new social media, traditional media coverage and urban space during the "Arab Spring". *Urban Studies*, 52(11).

Burns, A. na S. Mohapatra
2008 *International migration and technological progress*. Migration and Development Brief 4, World Bank, Washington D.C.

Castles, S.
2010 Understanding global migration: A social transformation perspective. *Journal of Ethnic and Migration Studies*, 36(19):1565–1586.

Czaika, M. na H. de Haas
2014 The globalization of migration: Has the world become more migratory? *International Migration Review*, 48(2):283–323.

De Witte, M.
2018 Stanford research explores the complexities of global immigration, from past to present, 18 April 2018, *Stanford News*. Inapatikana katika https://news.stanford.edu/2018/04/18/examining-complexities-migration/.

Faist, T. na N. Glick-Schiller (eds.)
2009 Migration, development and transnationalization: A critical stance. Papers in Special Section, *Social Analysis*, 53(3):106–122.

Fotaki, M.
2014 Narcissistic elites are undermining the institutions created to promote public interest. British Politics and Policy blog, London School of Economics, London, 21 February. Inapatikana katika https://blogs.lse.ac.uk/politicsandpolicy/narcissism-and-perversion-in-public-policy/.

Friedman, T.L.
2016 *Thank You for Being Late: An Optimist's Guide to Thriving in the Age of Accelerations*. Allen Lane, New York.

Goldin, I., G. Cameron na M. Balarajan
2011 *Exceptional People: How Migration Shaped Our World and Will Define Our Future*. Princeton University Press, Princeton.

Hall, K. na D. Posel
2019 Fragmenting the Family? The complexity of household migration strategies in post-apartheid South Africa. *IZA Journal of Development and Migration*, 10(2). Inapatikana katika https://doi.org/10.2478/izajodm-2019-0004.

* Viungo vyote vilikuwa vinafanya kazi wakati kazi ilichapishwa.

Hochschild, J. na J. Mollenkopf
2008 The complexities of immigration: Why Western countries struggle with immigration politics and policies. Migration Policy Institute, Washington D.C.

Ikenberry, G.K.
2018 The end of liberal international order? *International Affairs*, 94(1):7–23.

International Labour Organization (ILO)
2018 *ILO Global Estimates on International Migrant Workers – Results and Methodology*. 2nd edition. ILO, Geneva. Inapatikana katika www.ilo.org/wcmsp5/groups/public/---dgreports/---dcomm/---publ/documents/publication/wcms_652001.pdf.

International Organization for Migration (IOM)
2000 *World Migration Report 2000*. ILO, Geneva. Inapatikana katika https://publications.iom.int/books/world-migration-report-2000.

2003 *World Migration Report 2003: Managing Migration Challenges and Responses for People on the Move*. ILO, Geneva. Inapatikana katika http://publications.iom.int/books/world-migration-report-2003-managing-migration.

2017 *World Migration Report 2018*, IOM, Geneva. Inapatikana katika https://publications.iom.int/books/world-migration-report-2018.

Juskalian, R.
2018 Inside the Jordan refugee camp that runs on blockchain. *MIT Technology Review*, 12 April. *Napatikana katika* www.technologyreview.com/s/610806/inside-the-jordan-refugee-camp-that-runs-on-blockchain/.

Kapur, D.
2001 Diasporas and technology transfer. *Journal of Human Development*, 2(2):265–286.

Khadria, B.
2004 Human resources in science and technology in India and the international mobility of highly skilled Indians. Science, Technology and Industry Working Paper 2004/7, Organisation for Economic Co-operation and Development, Paris. Inapatikana katika www.oecd.org/officialdocuments/publicdisplaydocumentpdf/?cote=DSTI/DOC(2004)7&docLanguage=En.

King, R.
2012 Theories and typologies of migration: an overview and a primer. Working Paper. Malmö University, Malmö.

Koser, K.
2016 *International Migration: A Very Short Introduction*. Oxford University Press, Oxford.

Latonero, M., K. Hiatt, A. Napolitano, G. Clericetti na M. Penagos
2019 Digital Identity in the Migration & Refugee Context: Italy Case Study. Coalizione Italiana Libertà e Diritti Civili (CILD), Rome. Inapatikana katika https://datasociety.net/wp-content/uploads/2019/04/DataSociety_DigitalIdentity.pdf.

Mauldin, J.
2018 The age of change is coming, and these tech trends will drive economic growth. *Forbes*, 29 August. Inapatikana katika www.forbes.com/sites/johnmauldin/2018/08/29/the-age-of-change-is-coming-and-these-tech-trends-will-drive-the-next-decades-economic-growth/#6e78467131fd.

McAuliffe, M.
2016 How transnational connectivity is shaping irregular migration: Insights for migration policy and practice from the 2015 irregular migration flows to Europe. *Migration Policy Practice*, 6(1):4–10.

2018 The link between migration and technology is not what you think. *Agenda*, World Economic Forum, Geneva, 14 December. Inapatikana katika: www.weforum.org/agenda/2018/12/social-media-is-casting-a-dark-shadow-over-migration/.

Mishra, P.
2017 *Age of Anger: A History of the Present*. Farrar, Straus and Giroux, New York.

Muggah, R. na I. Goldin
2019 How to survive and thrive in our age of uncertainty. *Agenda*, World Economic Forum, Geneva, 7 January. Inapatikana katika www.weforum.org/agenda/2019/01/how-to-survive-our-age-of-uncertainty-muggah-goldin/.

Parsons, C.R., R. Skeldon, T.L. Walmsley na L.A. Winters
2007 Quantifying international migration, a database of bilateral stocks. In: *International Migration, Economic Development and Policy* (Ç. Özden na M. Schiff, eds.).

Rawnsley, A.
2018 Democracy is more fragile than many of us realised, but don't believe that it is doomed. *The Guardian*, 21 January. Inapatikana katika www.theguardian.com/commentisfree/2018/jan/21/democracy-is-more-fragile-than-many-of-us-realised-but-do-not-believe-that-it-is-doomed.

Ritholtz, B.
2017 The world is about to change even faster: Having trouble keeping up? The pace of innovation and disruption is accelerating. *Bloomberg Opinion*, 6 July. Inapatikana katika www.bloomberg.com/opinion/articles/2017-07-06/the-world-is-about-to-change-even-faster.

Sanchez, G.
2018 Critical perspectives on clandestine migration facilitation: An overview of migrant smuggling research. *Journal on Migration and Human Security*, 5(1):9–27.

Schwab, K.
2016 The Fourth Industrial Revolution: What it means, how to respond. *Agenda*, World Economic Forum, Geneva, 14 January. Inapatikana katika www.weforum.org/agenda/2016/01/the-fourth-industrial-revolution-what-it-means-and-how-to-respond/.

Skeldon, R.
2018 *International migration, internal migration, mobility and urbanization: Towards more integrated approaches*. Migration Research Series, Paper No 53, IOM, Geneva.

Stone, T.
2016 History tells us what may happen next with Brexit & Trump. *Medium*, 23 July. Inapatikana katika https://medium.com/@tswriting/history-tells-us-what-will-happen-next-with-brexit-trump-a3fefd154714.

Triandafyllidou, A.
2018 Globalisation and migration. In: *Handbook on Migration and Globalisation* (A. Triandafyllidou, ed.). Edward Elgar, Cheltenham.

United Nations Department of Economic and Social Affairs (UN DESA)
2003 *Long-Range Population Projections: Proceedings of the United Nations Technical Working Group on Long-Range Population Projections*. United Nations Headquarters, New York. Inapatikana at www.un.org/en/development/desa/population/publications/pdf/trends/population-projections.pdf.

2015 *Trends in International Migrant Stock: Migrants by Destination and Origin*. UN DESA, New York. Inapatikana katika www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/estimates15.asp.

2019a *International Migrant Stock 2019*. UN DESA, Population Division, New York. Inapatikana katika www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/estimates19.asp (accessed 26 September 2019).

2019b *World Population Prospects 2019*. Highlights. ST/ESA/SER.A/423, UN DESA, Population Division, New York. Inapatikana katika https://population.un.org/wpp/Publications/Files/WPP2019_Highlights.pdf.

United Nations General Assembly (UNGA)
2016 *New York Declaration for Refugees and Migrants*. A/RES/71/1, 3 October. Inapatikana katika www.un.org/en/development/desa/population/migration/data/estimates2/A_RES_71_1.pdf.

World Economic Forum (WEF)
2019 *Transformation Map on Migration* (curated by Marie McAuliffe, IOM). WEF, Geneva, Switzerland. Inapatikana katika https://intelligence.weforum.org/topics/a1Gb0000000LGr8EAG?tab=publications.